



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA ITIGI**



(BaruaazotezitumwekwaMkurugenziMtendajiWilaya)

Barua pepe: ded.itigidc@singida.go.tz

OfisiyaMkurugenziMtendaji (W),  
S.L.P. 70,  
**ITIGI.**

Kumb. Na.HW/ITG/E3/4/193

Tarehe: 11/09/2024

## **T A N G A Z O**

Msimamizi wa Uchaguzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Itigi anawatangazia Watumishi wa Umma wote nafasi za kazi kwa ajili ya shughuli za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa utakaofanyika tarehe **27 Novemba, 2024.**

**1. Nafasi zinazotangazwa:-**

- (a) Msimamizi wa Kituo
- (b) Afisa Mwandikishaji wa Wapiga kura

**2. Sifa zinazotakiwa**

- (a) Asiwe na dhamana au uongozi katika chama chochote cha siasa
- (b) Awe ni Mtumishi katika Utumishi wa Umma (Public Service).
- (c) Awe Mwadilifu.

**3. Namna ya kuandika barua**

- Barua zote ziandikwe kwa mkono
- Barua iandikwe majina kamili yanayotumika katika Utumishi
- Barua itaje nafasi ya kazi unayoomba.
- Barua itaje cheo katika Utumishi wa Umma
- Barua itaje kituo cha kazi
- Barua iwe na anuani kamili ikiwa na namba ya simu inayopatikana wakati wote
- Barua iambatishwe na maelezo binafsi (CV)
- Barua ziwasilishwe kwa mkono masijala ya wazi ya Mkurugenzi Mtendaji Itigi.
- Barua iandikwe kwa:  
    Msimamizi wa Uchaguzi,  
    Halmashauri ya Wilaya ya Itigi,  
    S.L.P 70, **ITIGI.**

**4. Mwisho**

Mwisho wa kupokea barua hizo ni tarehe 17 Septemba, 2024 siku ya Jumanne saa 9.30 Alasiri.  
Tangazo hili limetolewa na:

Ayoub J. Kambi  
MSIMAMIZI WA UCHAGUZI